KCU
QUALITY
COFFEE
Kagera Cooperative Union

MPYA

21/09/2026.

TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO KWA VITENDO (INTERNSHIP OPPORTUNITIES).

Kagera Cooperative Union (KCU) ni Muungano wa Vyama vya Ushirika 141 vilivyopo wilaya za Bukoba, Missenyi na Muleba Mkoani Kagera, Tanzania. KCU inajishughulisha na shughuli za kuratibu makusanyo ya kahawa ya wakulima wanachama wake wa vyama vya Ushirika, ikiwa ni pamoja na ununuzi, ukusanyaji, uchakataji, uuzaji wa kahawa katika masoko ya ndani na nje.

Katika kuimarisha uwezo wa vijana na kuwapatia uzoefu wa vitendo unaoendana na taaluma zao, **Kagera Cooperative Union (1990) Limited inakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na wanaohitaji fursa za mafunzo kwa vitendo (Internship)** katika Idara na vitengo vyake.

NAFASI ZINAZOTANGAZWA

1. MAFUNZO KWA VITENDO – UHASIBU NA FEDHA (ACCOUNTS & FINANCE)

Idadi ya nafasi: 2

Sifa za Mwombaji

- Awe amehitimu masomo ya **Shahada** katika Uhasibu, Fedha, Accounting and Finance au taaluma inayohusiana na hizo.
- Awe na uelewa wa msingi wa kanuni na taratibu za uhasibu.
- Awe na uwezo wa kutumia kompyuta.
- Uelewa wa matumizi ya mifumo ya uhasibu utapewa kipaumbele.
- Awe mwaminifu, mwenye nidhamu, bidii na utayari wa kujifunza.

MAJUKUMU

- Kusaidia katika utunzaji wa kumbukumbu za kifedha.
- Kusaidia katika kuingiza na kuhakiki taarifa za kifedha.
- Kusaidia katika uandaaji wa taarifa mbalimbali za uhasibu.
- Kusaidia katika ulinganishaji wa taarifa za benki na vitabu vya hesabu.
- Kusaidia katika utunzaji na upangaji wa nyaraka za kifedha.
- Kutekeleza majukumu mengine ya kitaalamu atakayopewa na msimamizi wake.

CamScanner

SIFA ZA JUMLA KWA WAOMBAJI

Waombaji wote wanatakiwa:

- Kuwa raia wa Tanzania.
- Kuwa na taaluma inayohusiana na nafasi wanayoomba.
- Kuwa na uwezo mzuri wa mawasiliano.
- Kuwa na uwezo wa kutumia kompyuta.
- Kuwa tayari kujifunza na kufanya kazi kwa bidii.
- Kuwa na uadilifu, nidhamu na uwezo wa kufanya kazi kwa kushirikiana na wengine.
- Kuwa tayari kufanya kazi katika mazingira ya biashara ya kahawa na shughuli za ushirika.

MUDA WA MAFUNZO KWA VITENDO

Muda wa mafunzo utazingatia mahitaji ya KCU, taaluma ya mwombaji na mahitaji ya Union pale inapohitajika.

Waombaji wanapaswa kutaja wazi katika barua zao:

- Nafasi wanayoomba.
- Muda wanaohitaji kufanya mafunzo.
- Taaluma waliyohitimu.

NYARAKA ZA KUWASILISHA

Mwombaji anatakiwa kuwasilisha:

1. Barua ya maombi.
2. CV yenye taarifa kamili za mwombaji.
3. Nakala za vyeti vya kitaaluma.
4. Nakala ya matokeo/transcript.
5. Nakala ya kitambulisho halali.
6. Anuani na mawasiliano ya wadhamini wawili.

NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo:

MENEJA MKUU
KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LIMITED
S.L.P. 5
BUKOBA.

Au kupitia barua pepe: kcubukoba@gmail.com.

CamScanner

MAMBO MUHIMU

- Mwombaji anatakiwa kutaja **nafasi/kitengo anachoomba** kwenye kichwa cha barua ya maombi.
- Maombi yasiyokamilika au yasiyoambatana na nyaraka muhimu hayatazingatiwa.
- Waombaji wanapaswa kuhakikisha kuwa taarifa wanazowasilisha ni sahihi na za kweli.
- Kagera Cooperative Union inazingatia usawa wa fursa kwa waombaji wenye sifa.
- **Ni waombaji watakaoteuliwa pekee ndio watakao taarifiwa.**

Mwisho wa kupokea maombi: Tarehe 05/10/2026.

Imetolewa na:

MENEJA MKUU
KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LIMITED
BUKOBA.

CamScanner